

## Maswali

1. Yesu na wanafunzi wake waliona nani kando ya barabara?
2. Kipofu alikuwa anafanya nini?
3. Yesu alisema eti kipofu au wazazi wake walikuwa na makosa?
4. Yesu alifanya nini kwa kipofu?
5. Yesu aliambia kipofu afanye nini?
6. Nini ilifanyika baada ya kipofu kuosha macho kwa birika ya Siloamu?
7. Umati ulifanya nini walipoona kipofu anaweza kuona?
8. Nani alimkuta yule mtu baadaye?
9. Yesu aliuliza yule mtu eti nini?
10. Yule mtu alisema nini?

## Majibu

1. Waliona kipofu.
2. Yule kipofu alikuwa akiomba.
3. Yesu aliwajibu kwamba yule kipofu wala wazazi wake hawajafanya makosa.
4. Yesu alitengeneza matope kwa mate yake na akaweka kwa macho ya kipofu.
5. Yesu alimwambia aende kwa birika ya Siloamu na aoshe macho yake.
6. Baada ya kipofu kuosha macho yake, yalipata kufunguka na yakaanza kuona.
7. Umati ulimuuliza maswali mengi sana. Hawakuamini kwamba Yesu ndiye alimfanya apate kuona.
8. Baadaye Yesu alipata yule kipofu.
9. Yesu aliuliza yule mtu kama anaamini Mwana wa Mungu.
10. Yule mtu alisema, “Bwana ninaamini.”

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



# 40 Yesu anaponya kipofu

## Marejeo

Yohana 9: 1 – 11 na 35 – 38

## Kiini cha somo

Kuonyesha vile Yesu alifanya mtu kipofu akaona na akaamini kwa Yesu

## Maneno maalum

- 40.1 Yesu + wanafunzi + kipofu + alizaliwa kipofu + mwombaji
- 40.2 Wanafunzi + makosa ni ya nani? + kipofu au wazazi + Yesu + hakuna wa makosa + onyesha uwezo wa Mungu
- 40.3 Yesu + kipofu + mate + tope + macho + enda uoshe + Birika ya Siloamu + nenda uoshe + macho yakafunguka
- 40.4 Furahi + pata Yesu + umati + maswali mengi + wapi Yesu + sijui
- 40.5 Yesu + kutana na mtu + una imini? + onana na Yesu + nina imini + furahi + onana na Yesu +rafiki wa Yesu

**40.1** Siku moja Yesu alikuwa anatembea barabarani na wanafunzi wake na akaona kipofu. Huyu mtu alikuwa hajawahi kuona kwa sababu alizaliwa kama kipofu. Huyu kipofu hakuweza kufanya kazi yoyote kwa hivyo alikaa barabarani akiomba pesa yakununulia chakula.



**40.2** Wanafunzi walipomuona huyo kipofu, walifikiria kwamba alizaliwa kipofu kwa sababu alifanya maovu. Au kuzaliwa kipofu, walifikiria ilikuwa adhabu kwa wazazi wake. Kwa hivyo waliuliza Yesu kama ilikuwa makosa yake au ya wazazi wake.

Yesu aliwajibu kwamba huyo mtu wala wazazi wake hawakufanya makosa. Alizaliwa kipofu ili uwezo wa ajabu wa Mungu uonekane kwa Yesu.

**40.3** Yesu aliita yule kipofu aje. Yesu alitema mate yake chini na akachanganya na ikawa matope. Alichukua hilo tope na kuweka kwa macho ya yule kipofu yaliyokuwa yamefungwa. Yesu alimwambia, “Nenda ukaoshe kwa Birika ya Siloamu.”

Haraka haraka, yule kipofu na fimbo yake akajikokota barabarani mpaka akafika kwa hiyo birika ya maji. Aliinama na akaosha matope kutoka kwa macho yake. Baada ya kuosha matope, macho yake yalifunguliwa na akaanza kuona. Ilikuwa maajabu namna gani!

**40.4** Alikuwa na furaha isiyo na kifani! Baadaye alirudi kutafuta mtu aliyemfanyia huu muujiza wa ajabu, lakini hakumpata. Watu wote walimwangalia kwa mshangao. Wakisema, “Huyu kweli ni mtu aliyekaa kando ya barabara akiomba.”

Muda wote watu walikusanyika kwake wakimuuliza maswali, pamoja wakizungumza. Aliwambia, “Ndiyo, ni kweli, mimi ndiye nilikuwa mwombaji kipofu.” Wakamuuliza, “Mbona sasa unaona?” Hawakuamini kwamba Yesu alimfanya apate kuona. Aliwambia akirudia rudia ni nini ilifanyika kwake. Walimuuliza, “Wapi huyu Yesu aliyekufungua macho?” Lakini hata huyu mtu hakujua.

**40.5** Baadaye Yesu alikutana na huyo mtu aliyezaliwa kipofu. Akamuuliza, “Unaamini kwa Mwana wa Mungu?”

Yule mtu alikuwa hajawahi kuona ingawaje alikuwa amesikia sauti yake. Kwa hivyo alijibu, “Yeye ndiye nani, Bwana? Niambia ili nipate kumwamini.”

Yesu alimjibu, “Sasa umemwona, ni kweli yeye ndiye unazungumza na yeye sasa hivi. Halafu huyo mtu akasema, “Bwana ninaamini.”

Huyo mtu alifurahi sana kwa sababu alikuwa amempata Yesu. Si kwamba alisikia sauti tu, lakini sasa ana MUONA. Yesu alikuwa rafiki wake na akafurahia.